



TAARIFA KWA UMMA

YAH: MALIPO YA KODI YA MABANGO YA MATANGAZO

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, ndugu Ally Machela, anapenda kuutaarifu umma kwamba, kodi za mabango ya matangazo ya huduma na biashara, zilizokuwa zinakusanywa na TRA, hivi sasa zitakusanywa na Manispaa.

Anawataka wafanyabiashara na watoa huduma mbalimbali za kijamii wenye mabango, wafike kwenye Ofisi ya Ujenzi ya Manispaa iliyopo Yadi, karibu na Ofisi ya Magereza Mkoa, kwa ajili ya kupata utaratibu na namba ya malipo (control number) ili waweze kulipia mabango yao.

Kwa wanaoanzisha biashara na huduma na wangependa kutengeneza mabango kwa ajili ya kutangaza huduma na biashara zao wanatakiwa kufika kwenye Ofisi ya Ujenzi ya Manispaa, iliyopo Yadi, karibu na Ofisi ya Magereza Mkoa, ili wapewe utaratibu na taarifa zao ziingizwe kwenye KanziData ya Manispaa.

Aina za mabango yanayopaswa kulipiwa ni pamoja na mabango yasiyowaka, yanayowaka, matangazo ya ukutani, matangazo ya kielektroniki, matangazo ya kwenye magari, maonesho ya mauzo sehemu ya biashara, vijarida vidogo vya matangazo na matangazo ya muda mfupi.

Aidha kodi hizi za mabango hulipwa mara moja tu kwa mwaka hivyo wahusika wote wanatakiwa kulipa kwa wakati ili kuepuka usumbufu.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini;
Manispaa ya Morogoro;
20.09.2023**